





© 2009 na World Missionary Press, Inc. Rose Stair Goodman, author. Mchoro wa jalada, Edwin B. Wallace. Meryl Esenwein, mchoro wa juu na katika ukurasa wa 10, 12, 14, 16, 27, 29, 39, 41, 42, 44, 46, 47, na 48.

## MUNGU ALIUMBA ULIMWENGU WETU NA VYOTE VILIVYO HAI 1

**"Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi."**
–Mwanzo 1:1

**"Kwa kuwa katika yeye vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi."** –Wakolosai 1:16a

**"Na mbarikiwe ninyi na Bwana, Aliyezifanya mbingu na nchi. Mbingu ni mbingu za Bwana, Bali nchi amewapa wanadamu."** –Zaburi 115:15, 16

Dunia ilikuwa nzuri wakati Mungu alimpa mtu. Soma kijitabu hiki ili uone ni nini kilitokea.

## 2 MUNGU ALITUUMBA



**"Mungu akasema, 'Na tufanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki . . . na nchi yote pia.' "**
–Mwanzo 1:26a

## MTU AKAWA KIUMBE HAI 3

**"Bwana Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai; mtu akawa nafsi hai*."** –Mwanzo 2:7

**"Bwana Mungu akasema, 'Si vema huyo mtu awe peke yake, nitamfanyia msaidizi.' Bwana Mungu akamletea Adamu usingizi mzito, naye akalala; kisha akatwaa ubavu wake mmoja, akafunika nyama mahali pake, na ule ubavu alioutwaa katika Adamu Bwana Mungu akaufanya mwanamke, akamleta kwa Adamu."**
–Mwanzo 2:18a, 21, 22

*Uzima maana yake tutakuwa mahali fulani kwa milele.

## 4 ADAMU NA EVA HAWAKUMTII MUNGU



Kamwe tusisikilize sauti ya Shetani.


**“Bwana Mungu akamtwaa huyo mtu, akamweka katika bustani ya Edeni, ailime na kuitunza. Bwana Mungu akamwagiza huyo mtu, akisema, ‘Matunda ya kila mti wa bustani waweza kula, walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika.’ ”** 5

–Mwanzo 2:15-17

NYOKA, PIA ALIITWA IBILISI AU SHETANI, ALIHOJI MAMLAKA YA MUNGU NA KUSEMA UONGO.

**“Nyoka akamwambia mwanamke, ‘Hakika hamtakufa,’ Mwanamke alipoona ya kuwa ule mti wafaa kwa chakula, wapendeza macho, nao ni mti wa kutamanika kwa maarifa, basi alitwaa . . . yake akala, akampa na mumewe, naye akala.”** –Mwanzo 3:4, 6

## 6 ADAMU NA EVA HAWAKUENDELEA KUKAA NDANI YA BUSTANI



**“Bwana Mungu akamtoa katika bustani ya Edeni, ailime ardhi ambayo katika hiyo alitwaliwa. Akaweka Makerubi . . . na upanga wa moto uliogeuka . . . kuilinda njia ya mti wa uzima.”** –Mwanzo 3:23b, 24b

## ILIKUWA SIKU YA HUZUNI KWA KIZAZI CHA BINADAMU WAKATI ADAMU NA EVA WALIPOTENDA DHAMBI 7



**“. . . Kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti; na hivyo mauti ikawafikia watu wote . . . . ”** –Warumi 5:12

**Kitu cha Kukumbuka**

**Kila mtu** amezaliwa katika asili ya dhambi na **siku fulani atakufa kwa sababu kifo kilikuja kwa njia ya dhambi.** (Soma Warumi 5:12 tena.)

## 8 MPANGO WA MUNGU KUTUOKOA KUTOKA DHAMBI ILIKUWA KUMTUMA MWANA WAKE PEKEE



Kuingia katika kizazi cha binadamu, Mwana wa Mungu lazima aje kama mtoto wa binadamu.

**“Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina lake Yesu, maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao.”**

–Mathayo 1:21

**“Maana katika Yeye** [Kristo Yesu] **unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili.”** –Wakolosai 2:9

## YESU NI MUNGU—KATIKA SURA YA BINADAMU 9

**“Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu.”** –Yohana 1:1, 14a

**“Hayo yote yamekuwa, ili litimie: ‘Tazama, bikira atachukua mimba, Naye atazaa mwana; Nao watamwita jina lake Imanueli;’ Yaani, ‘Mungu pamoja nasi.’ ”**

–Mathayo 1:22a, 23

**“Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, Tumepewa mtoto mwanamume; Na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake; Naye ataitwa jina lake, Mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani.”**

–Isaya 9:6

## 10 YESU KRISTO— DHABIHU YETU TAKATIFU

**“. . . Alimfanya kuwa dhambi . . . . ”** –2 Wakorintho 5:21



**“Yeye *hakutenda* dhambi.”** –1 Petro 2:22a

Hakuna dhabihu (sadaka) mtu angetoa iliyo TAKATIFU ya kutosha kuondoa dhambi.

**“Maana haiwezekani damu ya mafahali na mbuzi kuondoa dhambi.”** –Waebrania 10:4

Yesu ni Mwana Kondoo wa Mungu. **“Tazama, Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu!”** –Yohana 1:29b

## YESU ALITOA MAISHA YAKE KUTUOKOA SISI 11

Yesu alitundikwa katika msalaba wa mbao kwa sababu watu wakatili walimchukia. Lakini kifo chake ni mpango wa Mungu. Yesu kwa hiari Yake mwenyewe, alilaza chini maisha Yake kutuokoa mimi na wewe kutoka dhambi zetu.

Yesu alisema, **“Hakuna mtu aniondoleaye, bali mimi nautoa mwenyewe. Nami ninao uweza wa kuutoa, ninao na uweza wa kuutwaa tena.”** –Yohana 10:18a

**TUMEKOMBOLEWA KWA DAMU YA MWANA KONDOO WA MUNGU**


**“Nanyi mfahamu kwamba mlikombolewa si kwa vitu viharibikavyo, kwa fedha au dhahabu; . . . bali kwa damu ya thamani, kama ya mwana-kondoo asiye na ila, asiye na waa, yaani, ya Kristo.”** –1 Petro 1:18, 19

**HAKUNA DHABIHU NYINGINE ITAKAYOONDOA DHAMBI**

**“Kwa kutolewa mwili wa Yesu Kristo mara moja tu.”** –Waebrania 10:10b

**12** **“Tukiisha kuhesabiwa haki katika damu yake, tutaokolewa na ghadhabu kwa yeye.”** –Warumi 5:9b

**“Ee Yesu, nikumbuke utakapoingia katika ufalme wako.”** –Luka 23:42b



Mwizi huyu alimwamini Yesu na akaokolewa.

**“Amin, nakuambia, leo hivi utakuwa pamoja nami peponi.”** –Luka 23:43b

Mwizi huyu hakumwamini Yesu, hivyo hakuokolewa.

**“Kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi** [wasio watiifu kwa Mungu]**.”** –Warumi 5:8b

## WOTE WANAOAMINI KATIKA MWANA WA MUNGU WANAO UZIMA 13

**“Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.”** –Yohana 3:16

**“Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake; ambaye katika yeye tuna ukombozi*, yaani, msamaha wa dhambi.”** –Wakolosai 1:13, 14

*Ukombozi maana yake ni kununuliwa.

## 14 “AMEFUFUKA!”



**“Malaika akajibu, akawaambia wale wanawake, ‘Msiogope ninyi; kwa maana najua ya kuwa mnamtafuta Yesu aliyesulibiwa. Hayupo hapa; kwani amefufuka kama alivyosema. Njoni, mpatazame mahali alipolazwa.’ ”** –Mathayo 28:5, 6

## YESU ALITOKA MAUTINI 15

**“Na aliye hai; nami nalikuwa nimekufa, na tazama, ni hai hata milele na milele. Nami ninazo funguo za mauti, na za kuzimu.”** –Ufunuo 1:18

**“Na kwa sababu mimi ni hai, ninyi nanyi mtakuwa hai.”** –Yohana 14:19b

Kwa sababu Kristo alishinda mauti na anazo funguo za mautini, haitupasi kuogopa kifo.

**“Siku ya hofu yangu nitakutumaini Wewe.”** –Zaburi 56:3

(Tazama ukurasa 46 kwa ahadi za Mungu.)

**YESU ANAWEZA KUKUOKOA NA ANAKUOMBEA**

**“Bali yeye, kwa kuwa akaa milele. Naye, kwa sababu hii, aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa yeye; maana yu hai sikuzote ili awaombee.”** –Waebrania 7:24a, 25

## 16 WEWE NA MIMI TUNAWEZA KUWA NA UZIMA WA MILELE




**Njia ipi WEWE unaifuata?**

Yesu Kristo ni NJIA ya UZIMA wa milele pamoja na Mungu.

Ibilisi (Shetani) ni njia ya MAUTI ya milele.

Mvulana huyu amefanya chaguo njema ya uzima wa milele.

## WEWE UTAFANYA CHAGUO GANI? 17

**“. . . Chagueni hivi leo mtakayemtumikia. . . . ”**
–Yoshua 24:15

**“Basi chagua uzima, ili uwe hai, wewe na uzao wako.”**
–Kumbukumbu la Torati 30:19b

**YESU NI NJIA YA UZIMA WA MILELE**

**“Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo.”**
–Matendo 4:12

**“Mimi, naam, mimi, ni Bwana, zaidi yangu mimi hapana mwokozi.”** –Isaya 43:11

## 18 KWA NINI TUSIMCHAGUE YESU IKIWA TUNATAKA UZIMA WA MILELE?

**1.** ***Kristo ndiye aliyekuja.***

**“. . . Mimi nalikuja ili wawe na uzima . . . . ”** –Yohana 10:10



**2.** ***Kristo ndiye aliyetupenda na kufa kwa ajili yetu.***

**“Mwana wa Mungu . . . alinipenda akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu.”**
–Wagalatia 2:20b

Yesu alifanyika mtu, nyama na damu kama tulivyo sisi, **“ili kwa njia ya mauti amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani,** 19 **Ibilisi, awaache huru wale ambao kwamba maisha yao yote kwa hofu ya mauti walikuwa katika hali ya utumwa.”** –Waebrania 2:14b, 15


**3.** ***Damu ya Yesu pekee ndiyo itukomboayo kutoka dhambi zetu.***

**“Kwani ni hiyo damu ifanyayo upatanisho kwa sababu ya nafsi.”** –Mambo ya Walawi 17:11b

**“Na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote.”** –1 Yohana 1:7b

**“Ambaye katika yeye tuna ukombozi yaani, msamaha wa dhambi.”** –Wakolosai 1:14

20



**4.** ***Kristo ndiye aliyefufuka kutoka kwa wafu.***

**“Tukijua ya kuwa Kristo akiisha kufufuka katika wafu hafi tena, wala mauti haimtawali tena.”**
–Warumi 6:9

**“Tena alikufa kwa ajili ya wote, ili walio hai wasiwe hai tena kwa ajili ya nafsi zao wenyewe, bali kwa ajili yake yeye aliyekufa akafufuka kwa ajili yao.”** –2 Wakorintho 5:15

Yesu alisema, **“Na kwa sababu mimi ni hai, ninyi nanyi mtakuwa hai.”** –Yohana 14:19b

**5.** ***Lazima tuwe na Roho wa Kristo ndani yetu ili tufufuliwe kwa uzima wa milele*** *(kuishi kwa milele).* 21

**“Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu.”**
–Wakolosai 1:27b

**“Lakini, ikiwa Roho wake yeye aliyemfufua Yesu katika wafu anakaa ndani yenu, yeye aliyemfufua Kristo Yesu katika wafu ataihuisha na miili yenu iliyo katika hali ya kufa, kwa Roho wake anayekaa ndani yenu.”**
–Warumi 8:11

**HAKIKISHA ROHO WA KRISTO ANAISHI NDANI YAKO**

**“Lakini mtu awaye yote asipokuwa na Roho wa Kristo, huyo si wake** [siyo wake Kristo]**.”** –Warumi 8:9b

## 22 YESU ANAWAPENDA WATOTO WOTE



**“Akawakumbatia, akaweka mikono yake juu yao, akawabarikia.”**
–Marko 10:16

“Yesu ananipenda, hili nalijua, maana Biblia inaniambia hivyo.”

23

**“Bali Yesu akawaita waje kwake, akasema, ‘Waacheni watoto wadogo waje kwangu, wala msiwazuie, kwa kuwa watu kama hao ufalme wa Mungu ni wao.’ ”**
–Luka 18:16

**“Vivyo hivyo haipendezi mbele za Baba yenu aliye mbinguni kwamba mmoja wa wadogo hawa apotee** [kuteketea au kupotea milele]**.”** –Mathayo 18:14

Haijalishi wewe ni nani au wapi unaishi, Yesu anakupenda na alikufia. Yesu anataka upendo *wako*, pia. Unaweza kuonyesha upendo wako kwa Yesu kwa kumtii Yeye.

**“Mkinipenda, mtazishika amri zangu.”** –Yohana 14:15

**“Hata mtoto hujijulisha kwa matendo yake.”**
–Mithali 20:11a

## 24 NAMNA YA KUTAFUTA NJIA YAKO YA KWENDA KWA MUNGU

1. ***Kubali kwamba wewe ni mwenye dhambi*** *(angalia ukurasa 7)****.***

**“Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.”** –Warumi 3:23

2. ***Uje kwa Mungu kupitia Yesu Kristo.***

**“Kwa sababu Mungu ni mmoja, na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, Mwanadamu Kristo Yesu.”** –1 Timotheo 2:5

**“Kwa hiyo Yeye** [Yesu] **aweza kuwaokoa...wao wamjiao Mungu kwa yeye.”** –Waebrania 7:25a

Yesu alisema, **“Wala ye yote ajaye kwangu sitamtupa nje kamwe.”** –Yohana 6:37b


25

3. ***Kutubu dhambi zako.***

(Kutubu dhambi maana yake ni kuwa “na huzuni ya kutosha kuacha kutenda dhambi.”)

**“Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe.”** –Matendo 3:19a

**“Bwana hakawii...huvumilia kwenu, maana hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba.”** –2 Petro 3:9




4. ***Kiri dhambi zako kwa Yesu.***

(Kukiri maana yake ni “kumwambia au kumweleza.”)

**26** Katika mistari hapo chini andika au chapa mstari I Yohana 1:9a unaopatikana katika mikono inayoomba katika ukurasa 25.

________________________________________

________________________________________

________________________________________


5. ***Tupilia mbali dhambi zako.***

(Kusamehe maana yake ni “kuachilia, kutupilia mbali.”)

**“Afichaye dhambi zake hatafanikiwa; bali yeye aziungamaye na kuziacha atapata rehema.”** –Mithali 28:13

**“Jiepue na uovu, utende mema.”** –Zaburi 37:27a

27



**“Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani;...ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu.”**
–Waefeso 2:8, 9

6. ***Mwamini Yesu Kristo.***

**“Ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka.”**
–Warumi 10:9b

**“Mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka pamoja na nyumba yako.”**
–Matendo 16:31b

## 28 7. *Mpokee Yesu Kristo moyoni mwako na maishani.*

*Wewe* peke yako ndiwe utakayefungua moyo wako na kumwalika Yesu aingie ndani. Yesu alisema, **"Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami."** –Ufunuo 3:20



**"Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake."** –Yohana 1:12

## MWONGOZO WA KUOMBA 29

Ikiwa hujawahi kuomba na unahitaji msaada katika kuomba, unaweza kufuata maombi ya hapo chini kama mwongozo:



**Mpendwa Bwana Yesu,**
**Asante kwa kufa msalabani ili kuondoa dhambi zangu. Ninasikitika kwa maovu yote niliyotenda. Ninakuomba tafadhali ingia moyoni mwangu na kuishi milele. Ninakuamini sasa hivi utatakasa moyo wangu. Ninakupokea kuwa Mwokozi wangu na Bwana.**
**Katika Jina Lako Ninaomba, Amen.**

## 30 UKIWA NA YESU MOYONI MWAKO, UNAO UZIMA WA MILELE

**"Mungu alitupa uzima wa milele; na uzima huu umo katika Mwanawe. Yeye aliye naye Mwana, anao huo uzima."** –1 Yohana 5:11b, 12a


**"Yeye alisikiaye neno langu na kumwamini yeye aliyenipeleka yuna uzima... amepita kutoka mautini kuingia uzimani."** –Yohana 5:24b

Wakati mwili wako ukifa, wewe uko pamoja na Bwana (2 Wakorintho 5:8). **"Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu"** (Wakolosai 1:27b).

Ikiwa umemuuliza Yesu kusamehe dhambi zako, na kumwamini Bwana Yesu Kristo kuwa Mwokozi wako, andika jina lako hapa chini:

________________________________________

## NAMNA YA KUENDELEA KUMFUATA YESU 31



Soma mistari kutoka Biblia (Neno la Mungu) kila siku na kuyaficha moyoni kwa kuyakariri yaliyo muhimu ili yakusaidie. (Mengi yamo katika kijitabu hiki.)

**"Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho** [yale unayoamini]**, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki."**–2 Timotheo 3:16

## 32 ONGEA NA YESU KILA WAKATI KATIKA MAOMBI



***Umshukuru Yesu*** kwa mema yote katika maisha. ***Umtukuze*** kwa aliyokutendea na kuokoa roho yako. ***Omba kwa kila hitaji uliyonayo.*** Omba katika jina la Yesu.

**"Ya kuwa, tukiomba kitu sawasawa na mapenzi yake, atusikia."** –1 Yohana 5:14b

**"Mkimwomba Baba neno lo lote atawapa kwa jina langu."** –Yohana 16:23b

**"... Na kuombeana .... "** –Yakobo 5:16

**"Wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi."** –Mathayo 5:44b

## MAOMBI AMBAYO YESU ALIWAFUNDISHA WANAFUNZI WAKE 33

(Mwanafunzi ni mtu anayemfuata Yesu.)

Yesu aliwaambia wanafunzi wake kuomba namna hii:

**"Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe** [takatifu]**, Ufalme wako uje, Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni. Utupe leo riziki yetu. Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu. Na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu. [Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu, hata milele. Amina.]"** –Mathayo 6:9b-13

Maombi haya lazima yakaririwe. Waamini kila mara huomba kwa pamoja kwa sauti kuu maombi haya.

**34** **AMRI KUMI ZA MUNGU HUTUFUNDISHA NAMNA YA KUISHI**

(Kutoka, sura 20)

***Nne za Kwanza Zinahusu Upendo Wetu kwa Mungu***

1. **"Usiwe na miungu mingine ila mimi."**
2. **"Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu cho chote kilicho juu mbinguni. . . . Usivisujudie wala kuvitumikia."**
3. **"Usilitaje bure jina la Bwana, Mungu wako."**
4. **"Ikumbuke siku ya sabato uitakase."**

***Sita za Mwisho Zinahusu Upendo Wetu kwa Wanadamu***

**AMRI KUMI (ZINAENDELEA)** **35**

5. **"Waheshimu baba yako na mama yako."**
6. **"Usiue."**
7. **"Usizini"** (Uzinzi ni mapenzi ya kutokuwa mwaminifu kwa mume au mke.)
8. **"Usiibe."**
9. **"Usimshuhudie jirani yako uongo."**
10. **"Usiitamani nyumba. . . cho chote alicho nacho jirani yako."**

**UTIIFU KWA MUNGU HULETA MAJIBU KWA MAOMBI YETU**

**"Na lo lote tuombalo, twalipokea kwake, kwa kuwa twazishika amri zake, na kuyatenda yapendezayo machoni pake."** –1 Yohana 3:22

**36** **AMRI KUU MBILI**

***Upendo kwa Mungu***

1. **"Akamwambia, 'Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote. Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza.' "**
–Mathayo 22:37, 38

***Upendo kwa Watu***

2. **"Na ya pili yafanana nayo, nayo ni hii, 'Mpende jirani yako kama nafsi yako.' "** –Mathayo 22:39




Amri Zote Kumi (ukurasa 34 na 35) zimeingizwa ndani ya Amri Kuu Mbili.

**UPENDO NI AMRI KUU KULIKO ZOTE** **37**

**"Sura Kuu ya Upendo"**

(1 Wakorintho 13:1-8,13)

**[1]Nijaposema kwa lugha za wanadamu na za malaika, kama sina upendo, nimekuwa shaba iliayo na upatu uvumao. [2]Tena nijapokuwa na unabii, na kujua siri zote na maarifa yote, nijapokuwa na imani timilifu kiasi cha kuweza kuhamisha milima, kama sina upendo, si kitu mimi. [3]Tena nikitoa mali zangu zote kuwalisha maskini, tena nikijitoa mwili wangu niungue moto, kama sina upendo, hainifaidii kitu. [4]Upendo huvumilia hufadhili; upendo hauhusudu; upendo hautakabari; haujivuni; [5]haukosi kuwa na**

**38** **adabu; hautafuti mambo yake; hauoni uchungu; hauhesabu mabaya; [6]haufurahii udhalimu** [kosa], **bali hufurahi pamoja na kweli; [7]huvumilia yote; huamini yote; hutumaini yote; hustahimili yote. [8]Upendo haupungui neno wakati wo wote; bali ukiwapo unabii utabatilika; zikiwapo lugha, zitakoma; yakiwapo maarifa, yatabatilika.**

**[13]Basi, sasa inadumu imani, tumaini, upendo, haya matatu; na katika hayo lililo kuu ni upendo.**

**MUNGU NI UPENDO**

**"Mungu ni upendo, naye akaaye katika pendo, hukaa ndani ya Mungu, na Mungu hukaa ndani yake."** –1 Yohana 4:16b

**YESU ANAKUTAKA UWASHUHUDIE WENGINE** **39**



(nyumbani, shuleni, kanisani, popote)

Yesu alisema, **"Enenda zako nyumbani kwako, kwa watu wa kwenu, kawahubiri ni mambo gani makuu aliyokutendea Bwana, na jinsi alivyokurehemu."**
–Marko 5:19b

## 40 NAMNA YA KUMFAHAMU MTOTO WA KWELI WA MUNGU

**Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi.** –Yohana 13:35

**"Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi."** –Wagalatia 5:22, 23a

**MTOTO WA KWELI WA MUNGU HUWASAMEHE WENGINE**

**"Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi."** –Mathayo 6:14

**MAMBO 7 AMBAYO MUNGU HUYACHUKIA**

**"Macho ya kiburi, ulimi wa uongo, na mikono imwagayo damu isiyo na hatia; moyo uwazao mawazo mabaya; miguu iliyo myepesi kukimbilia maovu; shahidi wa uongo asemaye uongo; naye apandaye mbegu za fitina kati ya ndugu."** –Mithali 6:17-19

**MATENDO YA MWILI:** 41


**". . . Ndiyo haya, uasherati** [mapenzi kati ya wasio-oana]**, . . . ibada ya sanamu, uchawi, uadui, . . . hasira, fitina, . . . husuda, ulevi, ulafi, na mambo yanayofanana na hayo; . . . ya kwamba watu watendao mambo ya jinsi hiyo hawataurithi ufalme wa Mungu."** –Wagalatia 5:19-21

**" . . . Msidanganyike; waasherati hawataurithi ufalme wa Mungu, . . . wala wafiraji, . . . wala wevi, wala watamanio. . . .** –1 Wakorintho 6:9b,10a

**YESU AKUJAZE NA ROHO WAKE NA KUKUTAKASA**

**"Na baadhi yenu mlikuwa watu wa namna hii; lakini mlioshwa, lakini mlitakaswa, . . . jina la Bwana Yesu Kristo, na katika Roho wa Mungu wetu."** –1 Wakorintho 6:11

## 42 JEHANAMU NI YA HAKIKA




**(Soma Luka 16:19-26.)**

Hakikisha unamwamini Yesu Kristo. Ataweka jina lako katika Kitabu Chake cha Uzima.

**"Na iwapo mtu ye yote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto."** –Ufunuo 20:15

## YESU NI NJIA PEKEE YA KUFIKA KWA MUNGU 43

**"Mungu alitupa uzima wa milele; na uzima huu umo katika Mwanawe."** –1 Yohana 5:11b

**"Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu."** –Warumi 6:23

**"Amwaminiye Mwana yuna uzima wa milele; asiyemwamini Mwana hataona uzima, bali ghadhabu ya Mungu inamkalia."** –Yohana 3:36

**"Yesu akamwambia, 'Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi.' "** –Yohana 14:6

## 44 MBINGU NI MAHALI PA HAKIKA



Katika maono ya Yohana katika Ufunuo 21 aliona mbingu mpya na nchi mpya.

**" 'Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita.' Na yeye aketiye juu ya kile kiti cha enzi akasema, 'Tazama, nayafanya yote kuwa mapya.' "** –Ufunuo 21:4, 5a

Yohana pia aliona Mji Mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka kwa Mungu mbinguni. **"Mji ule ulikuwa wa dhahabu safi, mfano wa kioo safi. Na misingi ya ukuta wa mji ilikuwa imepambwa kwa vito vya thamani vya kila namna."** –Ufunuo 21:18b, 19a

## 45 YESU AMEENDA KUANDAA NYUMBA KWA WOTE WANAOAMINI KATIKA YEYE

**"Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu, niaminini na mimi. Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo, ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi mwepo."** –Yohana 14:1-3

**ELEZA KWA WENGINE HABARI HII NJEMA**

Yesu alisema, **"Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe."** –Marko 16:15b

**"Mwenye hekima huvuta roho za watu."** –Mithali 11:30b

## 46 AHADI ZA MUNGU KWA WATOTO WAKE

**"Sitakupungukia kabisa, wala sitakuacha kabisa."** –Waebrania 13:5b

**"Kwa kuwa atakuagizia malaika zake wakulinde katika njia zako zote."** – Zaburi 91:11



**"Wala hakuna mtu awezaye kuwapokonya katika mkono wa Baba yangu."** –Yohana 10:29b

**"Mimi nipo pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari."** –Mathayo 28:20b

**"Usiogope mambo yatakayokupata. . . . Uwe mwaminifu hata kufa, nami nitakupa taji ya uzima."** –Ufunuo 2:10


**"Nitasimama tena; nikaapo gizani, Bwana atakuwa nuru kwangu."** –Mika 7:8b

**"Niite, nami nitakuitikia."** –Yeremia 33:3a

## YESU ANAKUJA TENA 47

*Kila mtu* atafufuliwa kutoka kwa wafu.

**"Kwa maana saa yaja, ambayo watu wote waliomo makaburini wataisikia sauti yake. Nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima, na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu."** –Yohana 5:28b, 29



*Waliokufa katika Kristo* watafufuka kwanza.

**"Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele. Basi, farijianeni kwa maneno hayo."** –1 Wathesalonike 4:17

**"Kesheni, [ombeni], kwa kuwa hamjui wakati ule utakapokuwapo."** –Marko 13:33b

## 48 JINSI GANI YESU ATAKUJA?



**"Tazama, yuaja na mawingu; na kila jicho litamwona."** –Ufunuo 1:7a

Jihadhari na makristo wa uongo na manabii wa uongo.

**"Mtu akiwaambia, 'Tazama, Kristo yupo hapa,' au yuko kule, msisadiki. Wakiwaambia, 'Yuko jangwani, msitoke; yumo nyumbani,' msisadiki."** –Mathayo 24:23b, 26b

### YESU ATAKUJA HARAKA KATIKA MAWINGU YA MBINGU

**"Kwa maana kama vile umeme utokavyo mashariki ukaonekana hata magharibi, hivyo ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu. Ndipo mataifa yote ya ulimwengu. . . nao watamwona Mwana wa Adamu akija juu ya mawingu ya mbinguni pamoja na nguvu na utukufu mwingi."** –Mathayo 24:27, 30b

## ZABURI YA MCHUNGAJI

**(Zaburi 23)**

1 **Bwana ndiye mchungaji wangu, Sitapungukiwa na
kitu.** 2 Katika malisho ya majani mabichi hunilaza, Kando ya
maji ya utulivu huniongoza. 3 Hunihuisha nafsi yangu; na
kuniongoza Katika njia za haki kwa ajili ya jina lake.
4 **Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti,
Sitaogopa mabaya; Kwa maana Wewe upo pamoja
nami, Gongo lako na fimbo yako vyanifariji.** 5 Waandaa
meza mbele yangu, Machoni pa watesi wangu. Umenipaka
mafuta kichwani pangu, Na kikombe changu kinafurika.
6 **Hakika wema na fadhili zitanifuata Siku zote za maisha yangu; Nami nitakaa nyumbani mwa Bwana milele.**

The Bible text used is from the BIBLIA, 1970. The Bible Society in East Africa. (Alternate Kiswahili: Mistari za Biblia zilizotumika ni kutoka BIBLIA, 1970. Chama cha Biblia katika Afrika ya Mashariki.)

If you are interested in receiving additional studies of God's Word, write to the publisher:

**World Missionary Press, Inc.**
**P.O. Box 120**
**New Paris, IN 46553-0120 USA**



**Bure—Kisiuzwe** 2303 Kiswahili WTG